# AZIMIO LA ARUSHA
# MAJIBU KWA MASWALI

KAVAZI LA MWALIMU NYERERE
NYERERE RESOURCE CENTRE

# AZIMIO LA ARUSHA
# MAJIBU KWA MASWALI

**Julius. K. Nyerere**

**Kavazi Occasional Paper, No.5**
**2017**

Toleo la kwanza 2017
Chapisho la Pili 2018

© Kavazi la Mwalimu Nyerere

ISBN: 978-9976-9903-7-9

Kitabu hiki kimechapishwa kwa hisani ya Rosa Luxembourg Stiftung (RLS) inayofadhiliwa na Wizara ya Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo ya Kijerumani.

Kimechapwa na Inter Press of Tanzania Ltd.
Dar es Salaam.

# DIBAJI

Miezi miwili tu baada ya kupitishwa kwa Azimio la Arusha katika kikao cha Halmashauri ya Chama, TANU, mwishoni mwa Januari 1967, Mzee Kawawa aliwatangazia wabunge kwamba kama wana maswali juu ya Azimio wayawasilishe na yatajibiwa. Katika kuitikia wito huo wabunge waliwasilisha takriban maswali 21 ambayo yalijibiwa na Mwalimu Nyerere mwenyewe. Kama tujuavyo, Azimio la Arusha lilikuwa na mambo mawili makubwa (angalia chapisho la Kavazi liitwalo *Simulizi za Azimio la Arusha*, 2017). Mosi, ni utaifishaji wa njia kuu na nyeti za uchumi na, pili, utungwaji wa miiko ya viongozi wa serikali, mashirika ya umma na chama. Utaifishaji uliwagusa moja kwa moja mabepari wa nje ambao walikuwa wanamiliki viwanda, mabenki, bima, migodi ya madini na biashara ya jumla ya nje.

Walikuwemo pia mabepari wa ndani ambao wakati ule wengi walikuwa Watanzania wenye asili ya kihindi. Hao walikuwa wanamiliki viwanda vichache lakini zaidi vinu vya kusindika na kusaga nafaka. Utaifishaji haukuwapendeza mabepari wa nje na nchi zao ingawa wasingeweza kuupinga kwa sababu serikali aliwaahidi fidia. Kwa hivyo, mvutano ukawa kuhusu kiwango cha fidia na masharti ya ulipaji wake.

Ndani ya nchi, viongozi na wananchi walifurahia sera ya utaifishaji na waliipokea kwa mikono miwili. Lakini viongozi, sio wananchi, hawakupenda kabisa miiko ya uongozi, hususan, kile kifungu kilichowazuia kumiliki nyumba za kukodisha. Viongozi wengi, mara baada ya uhuru, walianza kujenga nyumba za kukodisha ili kujiongezea mapato. Hata katika kikao cha Halmashauri miiko ndiyo iliyowapa viongozi wengi shida, wakiwemo wanachama mashuhuri kama Mzee Rupia. Kulikuwa na kulaumiana na kunyoosheana vidole. Mjumbe mmoja alimshambulia sana Bibi Titi Mohamed akidai kwamba Bibi Titi alilipinga Azimio kwa sababu alikuwa anamiliki nyumba nyingi

tu. (Angalia kitabu cha Susan Geiger *Wanawake wa TANU*, 1997 uk 101). Malalamiko dhidi ya miiko ya uongozi yaliendelea kichinichini na yanajitokeza waziwazi katika maswali yaliyowasilishwa na wabunge. Takriban maswali yote yalikuwa juu ya masharti ya uongozi na hakuna hata moja lililohusu ujamaa.

Nini hasa mantiki ya miiko au masharti ya uongozi? Ni muhimu kuelewe vizuri mantiki ya miiko ya uongozi hiyo kwa sababu siku hizi wapo wachache wanaopindisha maana yake wakidhani kuwa maana yake yanaweza kulinganishwa na hoja za maadili ya uongozi na utenganishaji wa biashara na siasa. Kimuktadha na kimantiki, miiko ya uongozi ni sehemu kuu ya Azimio la Arusha na kwa hiyo mambo haya mawili hayawezi kutenganishwa. Hoja ilikuwa hivi: Azimio lilidhamiria kujenga nchi ya kijamaa, nchi ambayo haina matabaka ya wanaonyonya na wanaonyonywa ili hatimaye kila mtu aweze kuishi kwa jasho lake. Kwa hivyo, Azimio lilidhamiria kujenga nchi ya wakulima na wafanyakazi ambao ndiyo hasa wavujajasho.

Kwa kuwa ujamaa ndio ulikuwa sera ya Chama na serikali yake, basi viongozi wa chama na serikali ambao ndio walioamua kujenga nchi ya wakulima na wafanyakazi, hawana budi pia wawe wakulima au wafanyakazi. Wasiwe mabepari au makabaila kwa sababu huwezi ukahubiri ujamaa wakati wewe mwenyewe ni bepari. Kwa maana hiyo viongozi walipewa chaguo. Wakitaka kuendelea na vitendo vya kunyonya kwa maana ya kuwa na nyumba za kupangisha au biashara au hisa katika makumpuni ya kibepari, basi waiache ngazi ya uongozi. Hakuna mtu aliyekataliwa kuwa bepari isipokuwa alilazimishwa achague moja kati ya kuwa bepari au mjamaa. Ukitaka uongozi usiwe bepari. Ukitaka ubepari usiwe kiongozi.

Muktadha huu na mantiki hii ndiyo kiini cha hoja yangu kwamba miiko ya uongozi haihusiani hata chembe na maadili ya uongozi yanayozungumziwa siku hizi. Kwanza, miiko ya uongozi halikuwa suala la kimaadili. Hili lilikuwa ni suala la masharti ya kisheria. Pili, miiko ilichukuwa sura na sifa zake kutokana na dhamira ya kujenga ujamaa wakati maadili yanazungumziwa katika mazingira ya mfumo wa kibepari. Yaani, wanachoambiwa wanasiasa ni kwamba wawe na maadili ya kijamaa katika mfumo wa ubepari. Haiwezekani. Wala hoja hizi hazina mashiko. Mtu hazaliwi akiwa ni mjamaa au bepari, na kwa hivyo mtu hazaliwi na maadili. Mtu hupata maadili yake kutokana na mfumo uliopo. Kama wewe ni kiongozi mjamaa katika mfumo wa kibepari unapaswa kupinga mfumo huo na wala huwezi kukubali kuongoza mfumo ambao ni hasi kwa mtazamo wako.

Vilevile hoja za kutenganisha biashara na siasa mara unapoingia katika uongozi wa kisiasa haziwezi kuhalalishwa kwa kulinganishwa na miiko ya uongozi kwa mujibu wa Azimio.  Hoja za kutenganisha siasa na biashara kama umeteuliwa au kuchaguliwa kuwa kiongozi wa kisiasa zinajikita kwenye msingi wa mgongano wa maslahi (conflict of interest). Kwa hivyo, sharti kama hili linatekelezwa kwa hao wanasiasa kuweka mali na biashara zao katika trust, kwa maana ya kwamba wanapokuwa katika utawala hawahusiki kuendesha biashara zao.

Hata hivyo, mie ninashindwa kuelewa hili linaepushaje mgongano wa maslahi kwa sababu mali yako na biashara zako zinabaki palepale na pindi utakapomaliza uongozi wako utarudi kwenye biashara zako. Mfano mzuri hapa ni Makamu wa Rais wa Marekani mstaafu aitwaye Dick Cheney. Cheney alikuwa na uhusiano na kampuni ya mafuta ya Halliburton. Mnamo mwaka 2005 serikali ya Marekani ilipitisha sheria ya kuzuia makampuni ya mafuta yasiharibu mazingira lakini kutokana na ushawishi wa Cheney, ambaye alikuwa Makamu wa Rais, Kampuni


ya Halliburton ilisamehewa. Halliburton hiyohiyo ndiyo iliyopewa upendeleo katika kupata kandarasi ya miradi ya mafuta huko Iraq baada ya Marekani kuivamia Iraq na kumpindua na kumuua Saddam Hussein. Je, wanaotetea dhana ya kutenganisha siasa na biashara na kuzihalalisha hoja zao kwa kutumia hoja za Azimio hawatupotoshi? Kwanza, hoja zao hazilingani na miiko ya Azimio, pili, hata katika mfumo wa kibepari, hoja za kutenganisha siasa na biashara hazifui dafu katika uhalisia wake.

Madhumuni yetu ya kuchapisha kijitabu hiki ni, mosi, kuwakumbusha vijana wetu historia ya Azimio katika mwaka huu wa 50 tangu kuzaliwa kwake na pili, kuibua mjadala kuhusu mazingira ya leo na somo gani tunaweza kujifunza kutokana na Azimio la Arusha.

Issa Shivji

Mkurungezi, Kavazi la Mwalimu Nyerere

Mei, 2017.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

AZIMIO LA ARUSHA

MAJIBU KWA MASWALI

1967

KIMEPIGWA CHAPA NA MPIGA CHAPA MKUU WA SERIKALI

DAR ES SALAAM

# AZIMIO LA ARUSHA

## MAJIBU NA MASWALI

Katika kikao cha Bunge cha mwezi wa Aprili, 1967, Bwana Kawawa aliahidi kuwa, kama Wabunge Waheshimiwa wana maswali zaidi juu ya Azimio la Arusha, wakiyaleta tutakuwa tayari kuyajibu.

Tumepokea maswali mengi na tumejitahidi kuyajibu. Kwa bahati mbaya karibu maswali yote yanahusiana na sehemu moja tu ya Azimio la Arusha. Ni maswali juu ya masharti ya Uongozi. Hakuna hata swali moja juu ya Ujamaa na kujitegemea.

# MASWALI MENGINE JUU YA AZIMIO LA ARUSHA

YANAJIBIWA NA RAIS MWALIMU JULIUS K. NYERERE

**1. Kama mtu anauza nyumba yake ya pili, hizo fedha atazifanyia nini ikiwa haruhusiwi kuzinunulia hisa ili aweze kuvuna na kufaidi faida yake?**

Kiongozi ye yote wa TANU, Serikali au Chama kinachohusika, ambaye atauza nyumba yake aweza akaweka fedha zake katika Benki ya Biashara au ya Posta; aweza kununua dhamana za Serikali; au aweza kujiwekea akiba katika Chama cha Kujiwekea Akiba. Akitumia njia yo yote katika hizo zilizotajwa kujiwekea fedha zake atalipwa faida na kuifaidi mwenyewe.

**2. Azimio la Arusha limefanya thamani ya nyumba ianguke Dar es salaam. Pia watu hawapendi kununua wala kujenga nyumba. Ikiwa mtu kajitahidi lakini kashindwa kuuza nyumba zake katika muda wa miezi kumi na miwili uliotolewa, atafanyaje?**

Ni kweli kwamba kabla ya Azimo la Arusha watu fulani waliutumia upungufu wa majumba Dar es Salaam kwa kujenga nyumba kiisha wakaziuza au kuzipangisha kwa gharama kubwa kuzidi kiasi. Jambo moja zuri ambalo limekwisha fanywa na Azimio la Arusha ni kwamba bei za majumba zimeshuka na sasa ni za nafuu zaidi. Lakini japo kama zimeshuka zaidi haiwezekani nyumba yo yote iuzwe kwa bei ya chini zaidi kuliko gharama ya kuijenga. Nyumba zitaendelea kuuzwa kwa faida japo kama ni ndogo. Lakini hata kama faida hiyo ni ndogo, jambo la kukumbukwa ni kwamba anayeipokea faida hiyo kwa kweli hakuifanyia kazi yo yote. Alikuwa ni mmoja tu wa watu wachache waliopata bahati ya kupewa mkopo wa kujijengea nyumba. Asipopata faida kubwa sana hawezi kunung'unika kana kwamba kalifanya kazi Taifa na Taifa halikumlipa malipo ya haki kwa kazi aliyolifanyia. Kabla ya mtu yeyote kusema kuwa kashindwa kuuza nyumba yake tutapenda

kujua anataka kuiuza kwa bei gani. Ikiwa mtu kajenga nyumba kwa Shilingi laki moja na nusu, na anataka aiuze kwa laki nne ni dhahiri aweza atashindwa kuiuza.

Lakini ikiwa kweli mtu yeyote atashindwa kuuza nyumba yake Dar es Salaam au mahali pengine bado ziko njia za kujiondolea tatizo lake. Nyumba hiyo kwa kweli hivi sasa si yake. Itakuwa yake baada ya malipo ya mkopo wake. Kabla ya kumaliza malipo hayo ni nyumba ya Benki au Shirika lilipomkopesha fedha za kuijenga. Basi kama kashindwa kuiuza anaweza kuirudishia Benki au Shirika lilipomkopesha. Itakuwa ni juu ya serikali kuamua kama mtu yeyote aliyerudisha nyumba yake anastahili au hastahili kurudishiwa gharama fulani fulani kama za kiwanja au ramani ya jengo.

3. **Kama mtu kafanya kazi Kwa Waingereza; Na baada ya utumishi wa miaka 15 kachukua kiinua mgongo chake akajijengea nyumba ambayo anapangisha, ni haki kumwambia mtu huyu auze nyumba yake?**

Kama jamaa huyu hana nia yo yote ya kutaka kazi ya madaraka au ongozi katika Serikali, TANU au Shirika linalohusika itakuwa si haki hata kidogo kumwomba auze nyumba yake. Na wala hakuna mtu ye yote anayemwomba au atakayemwomba Mheshimiwa huyu kuuza nyumba yake. Lakini kama anataka uongozi katika TANU, Serikalini au katika Mashirika yanayohusika ni halali kabisa, na wala si haramu kamwe, kumwomba Mheshimiwa huyu angalao ajaribu kuishi kama 99.9 kwa mia ya wananchi ambao anasema kuwa angependa kuwaongoza au kuwatumikia. Yeye ana nyumba nzuri ambayo anaweza kukaa. Wao wana vibanda au hawana kabisa vibanda vyao wenyewe vya kuishi acha majumba ya kupangisha.

Azimio la Arusha linataka Kiongozi awe Mkulima au Mfanya kazi. Kwa nini? Ili kusudi ajue matatizo ya wale atakaowaongoza ambao ni wakulima na wafanya kazi. Kwa kuwa na nyumba nzuri ya kuishi

amekwisha kuwazidi wengi wa wananchi wenzake katika jambo moja la maana sana-nyumba. Kwa kuwa na nyumba ya kupangisha siyo kwamba atawazidi wananchi wenzake katika hatua ya pili, bali sasa atakuwa anawanyonya wananchi wenzake. Japo Mheshimiwa huyu alipata nyumba yake kwa jasho; sasa atakuwa anaitumia kama mrija.

Yafaa sana jambo hili lieleweke vizuri. Hata kama kodi anayotoza si kubwa, haizidi faida ambayo angepata kama angeziweka fedha zake katika Benki-kuna mambo mawili ya kufikiria. La kwanza ni kwamba Kiongozi atakuwa kajiweka katika hali ya kudhaniwa kuwa anaweza kwa faida yake mwenyewe kumpa au kumnyima mwananchi mwenzie mahali pa kukaa. Na huyu mwananchi mwenzie anaweza kufikiria kuwa hawezi kushindana na jamaa huyu maana yeye ni Kiongozi. Na jambo la pili ni kwamba mpangaji wake au watu wengine wanaweza wasiamini kwamba kodi anayotoza ni ya haki. Wataamini kwamba anamnyonya mpangaji wake japo kama hamnyonyi. Si jambo zuri hata kidogo kwa Kiongozi kujitia katika hali ambapo aweza kudhaniwa kuwa anawanyonya watu. Lazima iwe jitihada ya Kiongozi kujiweka katika hali ambayo ni dhahiri kwa mtu ye yote ila mwenda wazimu kwamba hanyonyi mtu.

**4. Kama mtu haruhusiwi kujenga na kupangisha nyumba; je, hii si kuzuia Waafrika kujenga majumba Dar es salaam na katika miji mingine na kuwaachia nafasi hii Wahindi na Wageni? Hili jambo ni la busara?**

Hili ni jambo la hila, na ni hila ambayo daima hutumiwa. Ni hila inayofanywa na kundi dogo kuutumia kama hirizi ukabila au ubaguzi wa rangi ili walio wengi wakihadaika wanaswe na hila hii, basi kundi lile la wachache liwanyonye badala ya wanyonyaji wa ukabila au rangi nyingine.

Azimio la Arusha, kwa kweli halizuii kabaila au bepari ye yote, akiwa mweupe, mweusi au miraba kuendelea na ukabaila au ubepari wake.

Azimio la Arusha halizuii kabaila au bepari Mwafrika kama ana uwezo na kama anapenda kujenga nyumba Dar es salaam au katika mji wo wote wa Tanzania na kuipangisha. Jambo ambalo linasemwa wazi na Azimio la Arusha ni kwamba ikiwa Mtanzania ye yote wa rangi yoyote atapenda kuwa kabaila au bepari, basi kwa kufanya hivyo atakuwa kajinyima mwenyewe kuwa kiongozi wa Chama cha Kijamaa au kushika kazi ya madaraka katika Serikali ambayo shabaha zake ni za ujamaa.

Waheshimiwa wanaouliza swali hili kwa njia hii ya kikabila-kabila na kirangi-rangi, ni Waheshimiwa ambao kwa kweli wangependa chama chetu kiwasaidie kuwa warithi wa wanyonyaji ambao wengi wao hapa kwetu walikuwa ni Waasia.

Azimio la Arusha ni Azimio la kuupiga vita unyonyaji; si azimio la kupiga vita unyonyaji wa rangi fulani, kwani unyonyaji hauna rangi. Anayenyonywa hajali kama mwenye mrija au mrija wenyewe ni mweusi, mweupe au manjano. Anachotaka ni kukata mirija, na hali yake haitakuwa bora zaidi kwa kuambiwa kuwa mirija ya kwanza ilikuwa myeupe na manjano lakini hii mipya ni myeusi na maji ya kunde. Mrija ni mrija tu, na halali yake kukatwa.

Kuna Waheshimiwa wengine ambao wangependa wawe washika mbili bila moja kuponyoka. Wangependa waendelee kuwa na nafasi ya kuwanyonya wananchi, na wakati huo huo wangependa haki na wadhifa wa kuwatumikia wananchi na kuwaongoza katika vita vyao vya kupigana na unyonyaji. Ukiwambia kuwa jambo hili haliwezekani, wanajaribu kutubabaisha kwa kutuambia kwamba wao ni weusi kama sisi! Wanatuambia "masikini ni weusi, na sisi ni weusi, kwa hiyo si vibaya tukiwanyonya: ni sisi kwa sisi!"

Kwa kweli hawasemi hivyo, maana wakiyasema wazi wazi hivyo wananchi watawatambua kwa haraka sana. Badala ya kusema hivyo hutubabaisha kwa kutaka tuamini kwamba mtu akinyonywa na mweusi mwenzie ni afadhali zaidi kuliko kama akinyonywa na mtu wa rangi nyingine.

Azimio la Arusha linahusu viongozi wote, bila kujali rangi zao. Linahusu madiwani wote wa Dar es salaam, Wahindi na Waafrika. Azimio la Arusha linalingana kabisa na kanuni ya kwanza ya TANU inayosema "Binadamu wote ni ndugu zangu………" Waheshimiwa wanaojaribu kuvuruga Azimio la Arusha kwa kutumia ukabila na ubaguzi wa rangi, kama Mheshimiwa aliyeuliza swali hili, ni watu ambao kwanza ni wanyonyaji na pili hawakubali kanuni ya kwanza ya TANU.

**5. Kama mtu haruhusiwi kutumia akiba yake ya fedha katika biashara au kujenga nyumba, atazifanyia nini fedha zake?**

Anaweza kujiwekea akiba yake katika Chama cha kujiwekea akiba, katika Benki ya Biashara, au Benki ya Posta au anaweza kununua dhamana ya Serikali. Akifanya hivyo fedha zake zitatumika kwa faida ya nchi nzima, mpaka hapo atakapozitaka, na nchi itafurahi kabisa kumlipa ujira kwa kuzitumia fedha zake.

**6. Watu waliojiwekea akiba katika Posta au Benki nyingine watafanyeje? Je, wataacha kufanya hivyo?**

Kwa nini waache? Tunataka wananchi wawe na mazoea ya kujiwekea akiba katika mabenki ili nchi yetu iweze kupata fedha za kutumia katika maendeleo. Ni kinyume kabisa kudhani kwamba watazuiwa kujiwekea akiba. Ukweli wenyewe ni kwamba watatakiwa na kushawishiwa kujiwekea akiba katika Benki ya Posta na Benki nyingine. Kujitegemea maana yake kwa upande wa fedha ni kwamba tuweze kujiwekea akiba sisi wenyewe na kutumia akiba hiyo kwa maendeleo yetu badala ya kutegemea akiba za watu wengine. Akiba wanazojiwekea watu wenyewe ni sehemu ya maana sana katika kujitegemea. Lakini akiba inayowekwa shimoni au uvunguni haina faida yo yote ila labda kwa mchwa au mende. Maana yule aliyejiwekea anaweza akaipoteza kabisa na wala nchi haitakuwa imeweza kuitumia kwa faida ya wote

Badala ya kuuliza swali hili kwa kweli ingefaa zaida kuuliza Serikali inafanya mipango gani ya kuwezesha wananchi kujiwekea akiba ndogo

ndogo. Na jambo bora zaidi, kuliko hata kuuliza swali, ni kusaidia wananchi wa kijiji chako kuanzisha chama cha kujiwekea akiba.

**7. Mtu atawezaje kuwatengenezea hifadhi mke na watoto wake atakapo kufa ikiwa haruhusiwi kuwaanzishia kibiashara au kuwaekea akiba?**

Azimio la Arusha linapinga unyonyaji. Na unyonyaji hauachi kuwa unyonyaji kwasababu shabaha yake ni kuhifadhi mke na watoto kama mnyonyaji akifa. Kila mwenye kuhodhi mamilioni huko Amerika atakuambia kwamba nia yake ni kuwaachia wanaye urithi mzuri na atakuwa anakuambia kweli. Ni vibaya kwa mtu mmoja kuwatengenezea maisha mazuri mke na watoto wake kwa kunyonya watu wengine, na wake zao na watoto wao. Mtu na–afanye kazi. Na mkewe na–afanye kazi. Na mtu na mkewe nawajiwekee akiba katika Benki ambako watalipwa ujira. Akiba hii itawasaidia wakati wa ajali au uzee. Huu ni utaratibu ambao kila mtu anauweza, ingawa kwa hali yetu ya sasa wengi wa wananchi hawana uwezo wa kujiwekea akiba yo yote katika Benki kwasababu pato lao lingali ni dogo mno.

Siku moja nchi yetu itaweza kuweka utaratibu wa malipo ya uzeeni kwa kila mtu; na kuwa na bima ya wajane na watoto yatima. Kwa sasa mambo haya yanawezekana kwa sehemu ndogo sana ya wafanya kazi wa mishahara na hasa watumishi wa serikali. Na maana ya swali hili, kwa kweli, ni kwamba kwa nini jamaa hawa hawa, pamoja na wanasiasa wachache, wasiruhusiwe kujijengea zaidi japo kama ni kwa njia za kunyonya watu wengine. Na hili ndilo jambo linalopingwa kabisa na Azimio. Azimio linamnyima kiongozi wa chama chetu au mtumishi wa wananchi haki ya kujijengea maisha yake na ya walio wake kwa kunyonya wale anaojidai kuwaongoza na kuwatumikia.

**8. Mtu atawezaje kuhakikisha kwamba akishakufa, au akiacha kazi, watoto wake wataendelea kupata elimu ikiwa haruhusiwi kutumia akiba yake kwa kujiongezea pato?**

Hii ni hila nyingine tena ya kujaribu kupendekeza unyonyaji kwa kutumia watoto na mahitaji yao kuwa hirizi nyingine. Kuna kiongozi gani Tanzania ambaye amekuwa anasomesha wanaye kwa fedha zake mwenyewe? Hata katika shule za kwanza ambazo bado wazazi hutakiwa walipe "ada" kwa masomo ya watoto wao, kwa kweli gharama ya elimu hulipwa na mlipa kodi. Mwaka 1965 jumla ya ada zilizopokelewa katika shule za kwanza ilikuwa kiasi Sh. 10,000,000/- lakini Serikali kuu ililipa Sh. 47,000,000/- na Serikali za mitaa Sh. 39,000,000/-. Hizi ni fedha za kodi, ambazo hulipwa na kila mtu, mwenye mtoto na asiye na mtoto; yule ambaye kapata nafasi shuleni, na yule ambaye mwanaye hakupata wala hatapata nafasi shuleni. Hiyo ni elimu ya kwanza. Katika shule za sekondari na Vyuo Vikuu gharama zote hulipwa na mlipa kodi. Wakati peke yake ambapo Watanzania hulipia elimu ya watoto wao ni pale wanapoamua kuwanunulia watoto wao nafasi maalum. Yaani ni wakati ambapo mtoto asipopata nafasi katika shule ya Sekondari, basi, zipo shule chache zinazoitwa "private" ambako ada ni za juu sana, na elimu mara nyingi ina walakini. Kama kabaila ye yote akipenda kulipa gharama hizi kwa ajili ya mwanaye, hiyo ni ada yake-na wala hazuiwi kufanya hivyo. Lakini kwa Kiongozi wa Chama cha Kijamaa kujaribu kupendekeza unyonyaji wa watu wengine eti kwa sababu utamwezesha kuwapatia wanaye nafasi maalum ni kinyume kabisa cha imani yetu. Ni wajibu wa Kiongozi wa TANU kutambua kwamba japo kama mzazi ni haki yake na maumbile kuwapenda watoto wake; lakini katika hali yake ya uongozi ana wajibu ule ule kwa watoto wote wa wale anaowaongoza.

### 9. Mtu atajitengenezeaje hifadhi ya uzeeni atakapokuwa ni mzee mno kulima?

Wengine anaowaongoza au waliomchagua kuwa Mbunge wanajitengenezeaje hifadhi ya uzeeni? Kwanini Kiongozi wa TANU awe tofauti hivyo na wale anaowaongoza? Kwanza yeye ana kipato kizuri. Kama ni Mheshimiwa Mbunge atakuwa kwa muda wa miaka mitano anapokea pato la Sh. 14,000/-kwa mwaka, bila kuongeza posho

zingine anazopokea. Pengine hakuna hata mtu mmoja miongoni mwa wale anaowaongoza au waliomchagua ambaye anapata pato kama hilo. Wengi wa wale anaowaongoza watajiona kuwa wana bahati ikiwa katika maisha yao yote wanaweza kupata pato ambalo yeye atalipata kwa muda wa miaka mitano-yaani Sh. 70,000/-

**10. Hali ya mwanasiasa haina uhakika. Leo ni Waziri, kesho si Waziri; leo ni Mbunge, baada ya miaka mitano si Mbunge; leo ni Katibu wa Mkoa au Katibu wa Wilaya, kesho hana kazi; leo ni Mwenyekiti wa Mkoa, au Wilaya au Mji kesho katupwa na wananchi kwenye uchaguzi. Je, Azimio la Arusha haliwaonei Viongozi hawa ikiwa litawazuia kutumia njia zingine kujitengenezea maisha yao ya baadaye?**

JIBU: NJIA GANI? Swali hili ni swali linaloulizwa zaidi na Viongozi kuliko swali jingine lolote; na ni swali chafu zaidi kupita mengine yote. Azimio la Arusha linasema kuwa kiongozi wa TANU atakuwa ni mkulima au mfanya kazi. Kabla ya kuchaguliwa kuwa Kiongozi atakuwa anayo kazi, au ya ukulima au ya kuajiriwa kwa mshahara au ya kujitegemea, kama vile seremala, fundi chuma sonara na kadhalika. Hiyo ndiyo kazi yake ya kupatia riziki leo na kumsaidia kujitengenezea maisha yake ya baadaye. Atakapoomba wananchi wenzie wampe shughuli ya uongozi (kwa mujibu wa Azimio la Arusha), moja litatokea baina ya mambo mawili: shughuli aitakayo yaweza ikawa ni shughuli ambayo itamzuia kuendelea na kazi yake ya sasa kwa sababu inahitaji wakati wake wote; au ni shughuli ambayo haitamlazimisha kuacha kazi yake, kwasababu haitahitaji wakati wake wote. Mathalani, Waziri au Katibu wa Wilaya hawezi kuendelea na kazi yake ya useremala au ukulima, hana budi aiache kabisa ikiwa anataka shughuli hiyo ya uongozi. Lakini balozi wa nyumba kumi, Mbunge au Mwenye Kiti wa Mkoa si lazima aache ukulima wake au useremala wake. Shughuli yake ya uongozi haichukui wakati wake wote.

Kiongozi wa aina ya kwanza hulipwa mishahara. Wengine, mikubwa wengine midogo; lakini wote hulipwa mishahara mizuri kwa hali yetu ya kitanzania. Mara nyingi mishahara hii humwezesha kiongozi kuwa na hali nzuri zaidi ya maisha kuliko kazi yake ya kwanza.

Kesho na kesho kutwa kiongozi huyu anaweza kuacha au kuachishwa uongozi wake. Ikiwa ataachishwa uongozi baada ya muda mfupi tu ataweza kurudia kazi yake ya zamani bila taabu kubwa; la, kama haitaki tena kazi yake ya zamani ataweza kutafuta kazi nyingine yo yote kama wafanyavyo wafaya kazi wengine. Maana isisahaulike kwamba kuacha kazi au kuachishwa kazi si jambo lililoletwa na Azimio la Arusha; ni jambo la kawaida katika nchi yetu. Na ni juzijuzi tu Serikali ya TANU ilipotunga sheria ya kuwalazimisha matajiri kuwalipa wafanya kazi malipo ya kuachishwa kazi. Lakini hata hivyo mfanya kazi aliyeachishwa kazi hana budi ajitafutie kazi nyingine. Na ingawa yeye ana malipo ya kuachishwa kazi, bali mwanasiasa hana, kwa kweli si malipo yawezayo kusemwa kuwa yatamsaidia kujitengenezea maisha yake ya baadaye. Kama tutakavyoona chini baadhi ya wanasiasa wanao uwezo mkubwa zaidi kujitengenezea maisha yao ya baadaye kuliko mfanya kazi wa kawaida.

Ikiwa ataacha au kuachishwa uongozi baada ya kuwa katika uongozi kwa muda mrefu mno na hataweza kurudia tena kazi yake ya zamani; bado atakuwa anaweza kutafuta kazi nyingine. Lakini zaidi ya hayo atakuwa amepewa na wananchi mshahara wa kutosha kujichukulia bima ya maisha. Kiongozi huyu, baada ya kuwanung'unikia wananchi, atakuwa ana wajibu wa kuwashukuru sana wananchi kwa kumwezesha kufanya hivyo maana wao wenyewe hawana mapato ya kutosha kuwawezesha kujichukulia bima za maisha.

Kiongozi wa aina ya pili ni wale ambao uongozi wao hauwalazimishi kuacha kazi zao za kawaida. Mathalani mtumishi wa Serikali anachaguliwa kuwa balozi wa nyumba kumi katika mtaa wake. Hatalazimishwa kuacha kazi yake ya kawaida kwasababu ubalozi

huu hautataka atumie wakati wake wote. Au mfanya kazi kiwandani anachaguliwa kuwa Diwani wa Baraza la Mji; au mkulima anachaguliwa kuwa Mbunge au Mwenyekiti wa Wilaya au Kijiji chake. Kiongozi huyu ataendelea na kazi yake ya siku zote; na kama hapana budi kupewa posho inayomwezesha kufanya hii shughuli mpya. Kiongozi huyu hawezi kusema kuwa uongozi wake unamzuia kufanya kazi yake ya kujipatia riziki na kujitengenezea maisha yake ya baadaye. Shida za viongozi zinawahusu watu, ni kweli. Lakini ikiwa ni shida zinazoweza kuwazuia kufanya vyema kazi yao ya uongozi. Ni kwaajili hiyo viongozi hulipwa mishahara.

Lakini baada ya kusema yote hayo tusisahau jambo kubwa hasa. Nalo ni hili, kwamba uongozi siyo kazi ya kujipatia riziki au kujitengenezea maisha ya baadaye. Tofauti ya uongozi na kazi nyingine ni kwamba katika uongozi kile kinachotakiwa ni ule uongozi wenyewe na matunda yake kwa umma. Shabaha ya uongozi tunaojaribu kuunda katika nchi yetu ni manufaa ya waongozwao siyo ya waongozao. Japo viongozi mara nyingi wanasahau, na hasa kwa sababu viongozi mara nyingi wanasahau shabaha hii ya uongozi, ilikuwa ni jambo zuri wakumbushwe na Azimio la Arusha siyo wazidi kusahaulishwa.

Ni kiongozi gani ambaye wakati wa uchaguzi waliwaambia wananchi wamchague ili ajitengenezee hali yake ya baadaye? Ni nani ambaye alipata kazi katika TANU, na awe katibu wa wilaya au katibu wa mkoa, kwa kusema kuwa anaitaka hiyo kazi ili ajitengenezee hali yake ya baadaye? Kila tunapotaka kazi ya kisiasa, japo ni ya kuchaguliwa kwa kura au kuteuliwa na wakuu, husema tunaitaka kazi hiyo ili tuweze kuwatumikia watu, kulinda haki zao, na kuwasaidia kutimiza mahitaji yao. Kiongozi ana haki gani, basi, mara baada ya kuipata nafasi hiyo kusema anataka kuitumia ili kujitengenezea maisha yake ya baadaye?

Swali hili linahusu kiini hasa cha Azimio la Arusha na shabaha ya TANU na Tanzania huru. Maana kwa kweli swali lenyewe linauliza kwa nini kiongozi asiruhusiwe kutumia nafasi yake, umaarufu wake, na dhamana

aliyokabidhiwa na wananchi wenzie, kwa kujitengenezea maisha yake ya baadaye. Mkulima wa kawaida hana nafasi ya kuweza kukopa fedha na kujijengea nyumba ya kupangisha ili ajipatie faida. Kwa nini kule kuwa Mbunge, mathalani, kuibadili hali hiyo? Maana ubunge ukiibadili hali hiyo ni kwamba Mbunge atakuwa amepata nafasi ya kunyonya kwasababu ya ubunge wake. Tulipokuwa tunapigania uhuru ni wangapi miungoni mwetu tulifuatwa na makabaila na mabepari na kuombwa tuwe wakurugenzi katika makampuni yao? Ni wangapi tulikopeshwa mapesa ili tujijengee majumba ya kukaa au ya kupangisha? Ni wangapi tulikopeshwa mapesa ya kununua mashamba au kuajiri vibarua? Kama sasa tumeyapata mambo haya tangu tumepata uhuru, ni kwa sababu mabepari na makabaila wanataka kutuingiza katika unyonyaji ili tuweze kuwa watetezi wa unyonyaji. Kwa kweli swali hili linaonyesha kuwa walianza kufaulu.

Viongozi wa TANU na serikali wangestahili kuwa na matumaini yale yale ya hali ya baadaye kama wakulima na wafanya kazi walipochaguliwa kuwatumikia. Lakini kwa kweli hali ya viongozi ni nzuri zaidi. Wakati tunapokuwa katika uongozi hulipwa mishahara mizuri zaidi kuliko mapato ya wale tuwaongozao. Twaweza tukajiwekea akiba na kulipwa faida. Tusipochaguliwa tena, au tusipopenda kugombania uchaguzi, au kama ikionekana kwamba hatuwezi tena kufanya kazi tuliyokuwa tukifanya, tutakuwa tumekwisha kujitengeneze hali nzuri zaidi kuliko wengi wa wale tunaowaongoza. Sasa hivi tunawaambia wasio na kazi mijini waende shamba wakalime; tunawaambia wakulima wafanye bidii zaidi na kutumia maarifa zaidi katika kulima. Tuna haki gani kuwaambia mambo haya wakulima na wafanya kazi wenzetu ikiwa wakati wetu ukifika na kuacha kusema na kuanza kutenda tunaanza kutapatapa?

Hakuna mtu anayezuiliwa na Azimio la Arusha kujitengenezea hali yake ya baadaye kwa kujijengea nyumba, japo ya kupangisha. Lakini hawezi kufanya hivyo na aendelee kuwa Kiongozi wa wananchi. Mtu halazimishwi kuwa Kiongozi wa siasa. Mtu akiona kuwa uongozi sasa hauna matumaini ya mlo ana hiari ya kuacha na kufanya kazi anayoona

kuwa itamsaidia kujitengenezea hali yake ya baadaye kwa kunyonya wananchi. Lakini kwa kweli sidhani kama wengi wetu wanaweza kufanya hivyo. Baada ya kuuvua uongozi watagundua kuwa hawawezi kujitengenezea maisha yao kwa kuwanyonya wananchi, kwasababu uongozi wenyewe ndio uliokuwa unawapa uwezo huo.

**11. Kama mtu hakufundishwa na wala hana mazoezi yo yote ya kilimo, au mtaji anaoweza kutumia kununua vyombo vya kulimia, mbegu, mbolea, n.k atawezaje ghafla kwenda kulima baada ya kuacha kazi au akisha kuwa mzee na ana mke na watoto wa kutunza?**

Hili sio tatizo la wanasiasa peke yao. Ni tatizo la watu wote ambao wamekulia mijini na kufanya kazi mijini, na ambao baadaye hujikuta hawana kazi. Na hata hivyo bado ni tatizo linalohusu sehemu ndogo sana ya wananchi wa Tanzania. Maana sehemu kubwa sana ya wananchi walio katika miji hivi sasa wamewahi kuishi mashambani.

Lakini tatizo lenyewe ni la kweli na lina majibu mbali mbali. Kwanza ingefaa kutamkwa wazi kwamba mtu ambaye ni mzaliwa wa mjini na mkulia mjini, na mfanya kazi mjini, ikiwa kwa muda atakuwa hana kazi, na wala si kwa makosa yake wenyewe, hawezi kutimuliwa mjini kama mhuni. Mtu wa namna hiyo ni wa kufikiriwa haraka nafasi ya kazi ikipatikana. Lakini ikiwa ni dhahiri kwamba hapana uwezekano kwa kumpatia kazi upesi hana budi ajaribu kujipatia riziki yake kwa kilimo mashambani. Wizara ya Kilimo ina vyuo vya kufundishia wakulima ambao hawana kisomo au ujuzi. Idara hiyo na wafanya kazi wake walioko Mikoani wakisaidia wakulima watafurahia sana kumsaidia mtu yeyote ambaye ana shida za kweli ya kutojua. Ofisi ya Wilaya itampatia ardhi, na kama hana jamaa wa kumsaidia itaweza pia kumsaidia kwa vitu kama vyombo vya kulimia, mbegu na chakula mpaka atakapopata mavuno yake ya kwanza. Wakuu wa Wilaya na Mikoa watakuwa na wajibu wa kuwasaidia watu wa aina hiyo.

Jibu moja la swali hili ambalo hatuwezi kulikubali ni kusema kwamba mtu wa namna hiyo ataruhusiwa kunyonya watu wengine. Anaweza kusaidiwa kujitegemea kwa njia kama hizo nilizozitaja. Lakini hawezi kusaidiwa kunyonya.

Lakini kwa kweli ni Watanzania wachache sana sana ambao wataweza kujikuta katika hali kama hiyo. Lingekuwa ni jambo la ajabu, kwa mfano, kwa kweli lingekuwa ni jambo la aibu, kama Mheshimiwa Mbunge wa sehemu ya mashamba hajui kabisa kulima. Ni dhahiri pia kwamba atajua misaada ambayo wakulima wanaweza kupata, maana kama hajui mambo hayo, sioni vipi ataweza kuwashawishi wakulima kuongeza mapato yao kwa kutumia ukulima wa kisasa. Na kama anajua mambo yote haya, basi siku atakapokuwa si Mbunge tena, atajua jinsi ya kupata mashauri na msaada anaohitaji.

**12. Maazimio haya ya Arusha kwa jumla ni mazuri, lakini je kutimizwa kwake hakufanywi haraka mno, tena bila fikara na mipango ya kutosha?**

Swali hili laweza likawa na ukweli kidogo ndani. Yawezekana kweli kwamba hatukufanya, au hatufanyi mipango ya matayarisho ya kutosha ili kuwezesha shabaha zote za Azimio la Arusha kutimizwa bila bughudha na bila makosa. Lakini huo ndio wajibu wa viongozi katika Chama Chetu na Serikalini. Ni wajibu wao kuona kuwa mipango inafanywa ya kutuwezesha kutekeleza vyema maazimio ya Arusha. Na tunaposema hivyo tunajitoa makosa sisi wenyewe, na ndivyo inavyostahili Viongozi kujisahihisha. Hatuna budi tufikirie shabaha ya Azimio la Arusha na maana ya kujitegemea. Na kila mmoja wetu ana wajibu kutimiza shabaha zetu. Mawazo hayo hivi sasa lazima yawe yakizungumzwa katika chama na katika Serikali. Kama jambo ni zuri basi yafaa litekelezwe vizuri, na upesi.

Lakini ubaya wa swali la namna hii ni kwamba laweza kutumiwa, na mara nyingi limetumiwa, kama kisingizio cha kutotimiza Azimio la

Arusha. Wenye Mabenki ni miongoni mwa wale wanaotumia hila hii. Hutuuliza, "Kwa nini hamkutuonya mapema ili tuanze kujitayarisha?" Mtu anaposema kuwa maazimio ya Arusha yanatimizwa kwa haraka mno maana yake ni nini? Serikali ikiisha kuamua kuchukua Mabenki, basi ama itayachukua au haitayachukua; au tutachukua hisa nyingi katika Makampuni fulani fulani, au hatuchukui. Kama huna kazi na wala hakuna dalili zo zote kuwa utapata kazi kesho, basi, ama utakwenda shambani ukalime kama Watanzania walio wengi wafanyavyo au utaendelea kuzurura mabarabarani. Katika njia panda hizi hapana ya katikati. Na Viongozi wamepewa muda ili kama wataamua kuendelea na uongozi wao, basi, wamepewa nafasi ya kuweza kusafisha yahitajiyo kusafishika. Lakini hawana budi waamue sasa kama wataendelea na uongozi au utawashinda.

Katika historia ya binadamu hila hii imetumiwa mara nyingi sana kupinga mabadiliko ya maana kwa kusema kuwa "Ni mazuri………… Lakini……" Na ni hila ambayo hutumiwa na wale ambao hawajambo na ambao ndio wasiopenda mabadiliko. Kwa hiyo utawasikia watu wakisema "Usawa wa binadamu ni jambo jema……..Lakini;" "kutokuwa na ubaguzi wa rangi ni jambo jema…..Lakini;" "kujali hali ya maskini ni jambo jema………Lakini." Na hatima yake ile "lakini" ndiyo hufaulu, ile sehemu ya "jambo jema" huendelea kuwa jambo jema lakini haitimizwi kamwe. Kwetu sisi katika Afrika kosa hilo la kutofanya mema ya dhahiri ni kosa kubwa zaidi, kuliko kosa lolote tunaloweza kufanya katika kutimiza jambo ambalo tumekwisha kukubali kuwa ni jambo jema.

**13. Wabunge wenye mishahara miwili walikatwaje mshahara wao wa Bunge bila kuonywa na kabla ile miezi kumi na miwili haijaisha?**

Kwa kweli tulitazamia Wabunge wenye mishahara miwili wataacha wenyewe mmoja wa mishahara hiyo mara baada ya tarehe 5 Februari. Kusudi la miezi kumi na miwili lilikuwa ni kuwawezesha hasa watu

wenye biashara na majumba kuyauza bila hasara. Nia yake hakuwa ni kuwapa Viongozi muda zaidi wa kuendelea kula fedha za wananchi. Huu ni mfano wa swali la hila ile ile "Jambo hili ni zuri… Lakini….." Ni mfano pia wa kutumia sheria ili kuua madhumuni ya sheria yenyewe. Kazi ya Viongozi wa Chama na Serikali ni kuwatumikia watu siyo kutafuta njia na hila za kulinda manufaa yao wenyewe. Wala Azimio la Arusha haliwaombi viongozi kujiumiza mno; linachotaka ni kwamba madhali wanayo mapato ya kutosha kuwapatia chakula, na makazi, basi na washughulike na mahitaji ya wananchi. Mshahara wa Mheshimiwa Mbunge si mbaya.

Lakini kwa kweli Mbunge ana haki kubaki na mshahara wake wa Bunge na kuacha ule mwingine ikiwa ule wa Bunge ndio mzuri zaidi. Na wakati huo ukifika atatakiwa atoe ushahidi kwamba hapokei ule mshahara mwingine. Kwa sasa ukweli wenyewe ni kwamba Mbunge anayependa kuendelea kukaa na Ubunge mpaka dakika ya mwisho ataendelea kupokea mshahara wake wa Bunge mpaka muda wa ruhusa uishe.

**14. Mkuu wa Mkoa wa Pwani alikuwa na haki gani ya kupitisha sheria ya kulazimisha watu kuchukua vitambulisho vya kazi? Si Bunge peke yake ambalo lina haki ya kutunga sheria katika Tanzania? Kama sivyo, kwa nini tuna Bunge?**

Hakuna mtu yoyote aliyepitisha sheria ya kulazimisha watu kuchukua vitambulisho vya kazi. Ni Bunge peke yake ambalo laweza kupitisha sheria kama hiyo. Kamati ya Dar es salaam ambayo Mwenyekiti wake ni Katibu wa Mkoa iliamua kuwa watu ambao wanazurura mjini bila kazi hawana budi warudi makwao. Kamati iliona kuwa litakuwa ni jambo zuri sana kwa wafanya kazi ikiwa watakuwa na kitambulisho cha kazi ili wasibughudhiwe bure. Na ili kuondoa au kupunguza vitambulisho vya uwongo itakuwa vema kama kitambulisho cha aina moja tu kitatolewa na Wizara ya Kazi kwa wenye kazi wote.

Na wala sivyo Dar es salaam peke yake ambayo imechukua hatua za kuondoa tatizo la watu wasio na kazi na wale wasiopenda kufanya kazi, na ambao hutegemea rafiki, majirani au uharifu wa sheria. Na wala Dar es salaam siyo mahali pa kwanza kuchukua hatua hizo. Miji mingine pia inajishughulisha na tatizo hili. Lakini Dar es salaam imevumishwa zaidi kwasababu ya ukubwa wa tatizo lake na hasa kwasababu ndipo penye magazeti na radio.

Kama waheshimiwa Wabunge wanadhani kuwa Halmashauri hizi zinafanya makosa fulani fulani kutimiza shabaha za Azimio la Arusha, ni juu yao kutoa maoni yanayoweza kusaidia. Wanaweza kuwashauri Viongozi wenzao njia bora zaidi za kutimiza shabaha hizo katika vikao mbalimbali vya huko huko Mikoani, wakishindwa wanaweza kutoa mashauri yao katika Bunge. Lakini tatizo hili lipo na kamati zimo katika kulitatua. Haziwezi kusubiri Bunge.

**15. Je, si jambo la hatari kuwavunja moyo watu wanaojaribu kuinua maisha yao? Jambo hili halitawavunja nguvu, kuwakatisha tamaa, na kuleta uvivu?**

Wamenyimwa nini hata wavunjike moyo? Azimio linasema wazi wazi kabisa kwamba watu hawana budi wafanye kazi ili kujipatia riziki zao, na kwamba ni wajibu wa Jumuia kuona kuwa wanalipwa malipo ya haki kutokana na kazi yao. Kufanya hivyo kunawavunjaje moyo watu wanaojaribu kuinua maisha yao? Shabaha moja ya Azimio la Arusha ni kufanya jasho na pato yalingane zaidi; yaweza ikawa kutakuwa na utaratibu wa kuona mtu asiyefanya kazi sawa sawa ataachishwa kazi au atapata pato dogo zaidi kuliko yule anayefanya kazi yake vizuri. Lakini hizi ni njia tu za kujua pato la haki ni nini. Lakini si njia za kumvunja moyo mtu anayejaribu kuinua maisha yake kwa kufanya kazi.

Lakini ni kweli kabisa kwamba Azimio la Arusha linamfanya Kiongozi wa TANU na Serikali kupata taabu zaidi akijaribu kuinua maisha yake kwa kunyonya watu wengine. Hiyo ndiyo shabaha yake. Mtu anaweza

“kuinua maisha yake” kwa wizi au unyang’anyi. Hatumruhusu afanye hivyo. Je, kwa kumzuia kuiba au kuvunja majumba huwa tunamvunja moyo au kumkatisha tamaa? Yawezekana! Lakini ni haki yetu kufanya hivyo. Kiongozi anayejinenepesha kwa jasho la wengine si tofauti sana na mwizi; maana huwa anajidai kwamba anawatumikia wananchi, kumbe kwa kweli anatumia imani yao kujiongezea pato lake na kupunguza la kwao.

Hili sio jambo la mzaha. Mtu anayekopa fedha za Serikali anakopa pesa zilizotokana na kodi za wananchi. Akatumia fedha hizi kujenga nyumba Magomeni na kupangisha ili apate faida; mpangaji wake ambaye ni mmoja wa walipa kodi–anafanya mambo mawili. Kwanza kamwezesha huyu jamaa kupata mkopo; pili anamlipa sasa kwasababu kaweza kukopa fedha na kujijengea nyumba ya kupangisha. Kama jamaa yule asingekopa fedha zile Serikali yenyewe ingeweza kuzitumia kujenga nyumba nyingine. Yule mpangaji bado angepanga nyumba hii ya Serikali, lakini asingelipa kodi ya nyumba kubwa mno. Na serikali ingeliweza kuitumia hiyo kodi yake kusaidia kujenga nyumba nyingine au kufanyia shughuli nyingine ambayo ingeleta manufaa kwa walipa kodi kwa jumla. Lakini mtu nafsi anapokusanya kodi hiyo ni yeye nafsi anayoitumia kwa faida yake mwenyewe na jamaa yake.

Inasemekana kuwa matumaini haya ya kupangisha na kupata faida ndiyo hufanya watu waweze kujenga majumba. Vyema, ikiwa mtu atatumia fedha zake mwenyewe kujijengea hiyo nyumba ya kupangisha. Lakini ni Viongozi wangapi katika TANU au katika Serikali watakuwa wamejiwekea akiba ya kutosha kujijengea majumba ya kupangisha, na mengine ya kuishi wenyewe? Na hata hivyo kwanini aachiwe kutumia fedha hizo kwa njia hiyo? Jibu atakalotoa ni kwamba anazo fedha za kurithi au kwa njia nyingine –na atataka mtu mwingine amlipe kodi kubwa sana ya kupanga ikiwa anataka mahali pa kuishi. Huyu ni kiongozi wa TANU au Serikali ambaye atakuwa kwa kweli anasema “Jumuia imekadiria malipo ya haki kwa fedha zangu na inanilipa. Lakini siridhiki. Kwa hiyo badala ya kuweka fedha zangu katika Benki,

nitajenga nyumba ili nijipatie faida kubwa zaidi." Kwa kufanya hivyo huyo jamaa anaweza akawa anafanya kitendo ambacho ni halali kwa mujibu wa sheria za nchi. Lakini hatakuwa anaishi kwa kufuata kanuni za Chama anachojidai kuwa anakiongoza.

**16. Kama Azimio la Arusha likitimizwa hasa kama linavyokusudiwa, juhudi za kazi au elimu ya juu n.k itatuzwa tuzo gani?**

Tuzo la juhudi ya kazi ni mshahara wa haki. Na watu wenye elimu ya juu nao hupata mishahara mikubwa zaidi kuliko wale ambao hawana elimu kama hiyo. Lakini mshahara huo unatazamiwa uwe ni mshahara wa haki; na lazima ufanane kidogo na mapato ya kawaida katika nchi yetu.

Katika nchi tunayojaribu kujenga gharama za elimu zitalipwa na Jumuia nzima. Na kwa hiyo Jumuia itakuwa inayo haki ya kudai malipo ya haki kutoka kwa watu ambao itakuwa imewaelimisha. Hata hivi sasa na hata wakati wa mkoloni sehemu kubwa ya elimu inalipwa na Jumuia. Wazazi wa baadhi ya jamaa wenye elimu walilipa ada kidogo kwa elimu ya watoto wao. Mwaka 1960 Serikali Kuu ililipa £1,360,000 kwa elimu ya kwanza ya Waafrika na Serikali za mitaa zililipa £341,000. Elimu ya kati iligharimu £848,000, na elimu ya sekondari £254,000. Fedha hizi zililipwa na Jumuia nzima –yaani mlipa kodi-ada za wazazi mbali. Maana yake ni kwamba tangu elimu ya kisasa ianzishwe katika nchi yote gharama zake zinakuwa zikilipwa na Jumuia nzima. Hapana mtu yeyote mwenye elimu ambaye ataweza kusema kuwa hakusomeshwa na nchi nzima, bali kasomeshwa na wazazi wake.

Mtu ye yote anayeona kuwa Azimio la Arusha linafanya elimu ya juu iwe haina faida , hana haja ya kupokea elimu hiyo. Akipatiwa nafasi ya kuingia katika shule ya sekondari, chuo kikuu au chuo cho chote cha juu, anaweza kusema, "La, mimi sitaki. Elimisheni mtu mwingine; maana ujamaa wenu haulipi malipo mazuri kwa watu wenye elimu ya juu; na mimi naona ni afadhari nikae bila elimu hiyo, kuliko kuipata na kuitumia kijamaa."

## 17. Azimio la Arusha lina matumaini gani kwa vijana?

Azimio la Arusha linamwahidi kijana nafasi ya kufanya kazi kwa faida yake mwenyewe, jamaa yake na nchi yake. Linamlinda asinyonywe na mtu ye yote, na linamnyima haki ya kunyonya wengine. Linamwahidi nafasi ya kutumikia Jumuia yake, Na nafasi ya kuheshimiwa kwasababu ya utumishi wake. Linamnyima nafasi ya kuwa kupe juu ya umma, na hasa kama anajidai kuwa ni kiongozi.

Kwa vijana wa nchi yetu hakuna kitu bora kama Azimio la Arusha. Linawapa nafasi ya kutumikia nchi yao bila kuhatarisha nafasi yao ya kujipatia riziki. Watalitumikia taifa lao kwa kufanya kazi, na kwa kazi yao watalipwa pato la haki. Kijana ye yote ataweza kuishi kirafiki na kijamaa na watu wengine wote badala ya kujaribu kushindana nao kwa mali kwasababu wao wanajaribu kumzidi au kumnyonya.

Kijana atataka nini zaidi? Hicho ndicho vijana wa dunia nzima wakitakacho. Ni makatili tu ambao hufurahi kwa kusikia kuwa vijana wenzao wana njaa na wagonjwa, au hawana pa kulala ili wao waishi kwa anasa. Lakini vijana wa kawaida hawana moyo huo wa kikatili. Wao hupenda kupambana na matatizo; na wakisha kulielewa tatizo hawakawii kuitika mwito wa kupambana nalo. Kazi yetu sasa ni kuwaeleza maana ya wito wa Azimio la Arusha na juu ya Ujamaa na Kujitegemea.

## 18. Ni haki kushusha chini baadhi ya watu kwasababu ya kutaka kuinua hali za watu wengine?

Kama jamaa mmoja kastarehe juu ya lundo la mahindi na mwenziye anakula mizizi kwasababu hana chakula bila shaka itakuwa ni haki kumpunguza wa kwanza lile lundo lake ili wa pili apate chakula cha maana.

Lakini swali hili lina uhusiano gani na Azimio la Arusha? Azimio la Arusha linasema kiongozi ye yote hatarususiwa kunyonya watu; kwamba ni lazima taifa letu lijitegemee; na kwamba tutajitahidi kujenga

Taifa letu katika msingi wa usawa wa binadamu. Kiongozi anashushwaje chini anapoambiwa kuchagua baina ya kuishi kibepari na kushika kazi ya madaraka katika nchi ya kijamaa?

**19. Je, ni haki kuondoa picha za viongozi wa dini katika sehemu za hadhara kwa sababu viongozi hao ni wageni nasi twataka kujitegemea?**

Kuonyesha au kutoonyesha picha za viongozi wa dini katika sehemu za hadhara hakuna uhusiano wo wote na Azimio la Arusha wala kujitegemea. Uhuru wa dini ni msingi mmoja wa Katiba yetu; siasa yetu ya ujamaa haiubadili hata kidogo. Mtu hawezi kuwang'ang'aniza wengine dini yake. Lakini kila mtu ana haki ya kuabudu apendavyo na hakuna atakayejali kama kiongozi wa dini yake ni mweupe, mweusi au manjano, yu hai au marehemu.

**20. Mtu atawezaje kumwelimisha mwanae awe daktari au wakili kwa kutumia mshahara wa wastani wa mtumishi wa Serikali, Mbunge au Kiongozi, ikiwa haruhusiwi kujiwekea akiba na kujiongezea pato? Na kama hawezi kufanya hivyo tutapata wapi madaktari na mawakili?**

Gharama ya kumweka mwanafunzi mmoja katika Chuo Kikuu cha Afrika Mashariki ni Sh. 20,000/- kwa mwaka. Nchi yetu ingepata madaktari wangapi kama tungeacha wazazi ndio wawalipie watoto wao kwa muda wa miaka 7 ya kusomea udaktari? Na tungehakikishaje kwamba jamaa wenye uwezo wa kulipa ada kubwa kama hizo watakuwa pia wamejaliwa kupata watoto wenye akili za kutosha kusomea udaktari? Utajiri na akili si mtu na mwanaye.

Swali hili linatokana na kutojua gharama ya elimu, au ni hila tu ya kujaribu kuwadanganya wananchi. Hapana mtu ye yote katika nchi yetu ambaye kamwelimisha mwanaye kuwa daktari. Baadhi wamelipa ada ambayo imesaidia kuelimisha watoto wao. Basi. Lakini raia wengi wa Tanzania sasa hawalipi hata ada hizo.

Kanuni ya kushikilia ni kwamba elimu ya juu haina budi wapewe wale ambao wataweza kuipata na kuitumia kwa faida ya nchi nzima. Na njia bora ni kumpa nafasi kila mtoto wa Tanzania bila kujali mapato ya wazazi wao. Hatujafikia hali hiyo mpaka sasa kwa sababu nusu nzima ya watoto wetu hawapati nafasi ya kusoma. Lakini kutokana na wale waliopata nafasi ya kusoma lazima tuchague watoto wa kupata elimu ya juu kwa kufuata kanuni hii. Hatuwezi kumpa nafasi mtoto kwa sababu baba yake au mama yake ni tajiri, au kwa sababu baba yake au mama yake kasaidia sana maendeleo ya taifa letu.

**21. Mikoa itawafanyia nini wasio na kazi na wahalifu wa sheria wanaorudishwa mikoani kutoka mijini? Watu hao wasipopewa chakula na kazi, hii haitazidisha uvunjaji wa sheria? Ni haki kumwongeza mkulima mzigo huu wa wasio na kazi na wahalifu wa mijini?**

*Kwanza, wasio na kazi*. Watu wasio na kazi twaweza kwanza kuwagawa katika mafungu mawili. Fungu la kwanza ni wale ambao wametoka mashamba wakaja mjini kutafuta kazi wakakosa kazi. Fungu la pili ni wazaliwa wa mjini.

Na fungu la kwanza tunaweza pia kuligawa katika mafungu mengine mawili. Kwanza fungu la wale ambao wana jamaa zao na ardhi ya kutosha kule wanakotoka. Hawa wanaweza kurudi kule mashamba na na kupokelewa na jamaa zao na kulima kama walimavyo Watanzania wengine. Watasaidiwa na Serikali kama mkulima mwingine ye yote anavyosaidiwa. Hawatapewa msaada maalum, kwa sababu hawana tofauti na wakulima wengine na ambao hawapewi misaada maalum na Serikali.

Fungu la pili ni wale ambao wametoka mashamba, wanakubali kulima, lakini kule wanakotoka hawana jamaa, au wana jamaa lakini hakuna ardhi Mathalani, Mchagga wa Kilimanjaro anaweza awe hana ardhi kule nyumbani. Kadhalika mzaliwa wa mjini ambaye hana uwezo

wa kujisaidia mwenyewe. Hawa wanahitaji misaada. Ni wajibu wa Serikali kuwasaidia kupata ardhi, vyombo vya kutumia, mbegu, mbolea, chakula, n.k mpaka hapo watakapoweza kujitegemea. Serikali itaweka fungu la fedha kwa shughuli hii. Mwananchi ambaye anayo nia safi kabisa ya kulima, lakini hana ardhi, hana jamaa, au uwezo wa kujisaidia mwenyewe amjulishe tu Katibu wa Wilaya yake na mipango ya kumsaidia itafanywa.

*Pili, wavunja sheria.* Wavunja sheria ni tatizo po pote walipo. Wakiwa mjini ni tatizo; wakiwa mashamba ni tatizo. Lakini mara nyingi huwa hawafanyi shughuli zao hizo nyumbani kwao ambako wanajulikana na vitendo vyao vinajulikana. Ni rahisi zaidi kwao kujificha mijini ambako wanaweza kuvunja majumba au kufanya mambo mengine ya uhalifu bila kukamatwa. Wakirudishwa makwao na halafu wakazidi kuvunja sheria ni rahisi zaidi kwa polisi kuchukua hatua zinazotakiwa kwa sababu kule vijijini jamaa hao wanajulikana.

Lakini tunachotaka ni kuwapa nafasi mpya jamaa hao. Mijini wamekuwa na matumaini kwamba huenda kesho, au juma lijalo watapata kazi. Wakirudi mashambani watatambua kuwa hawana budi wajipatie jambo riziki yao kwa kufanya kazi. Wengi wana makwao. Na kwa kweli jambo linafanyika ni kuwafanya watambue ukweli: nao ni huu, kwamba njia ya kujipatia chakula na mahali pa kulala katika Tanzania, na kujipatia pato zuri, ni kufanya kazi shambani.

Kuwarudisha watu mashambani ni tatizo kubwa na utatuzi wake si rahisi. Mafanikio ya Watanzania wote, wa mijini na wa mashamba, msingi wake ni kujitegemea kwa nchi yetu na kujitegemea kwa kila mwananchi. Sidhani kama tutawasaidia wakulima mashamabani kwa kuzidisha na kung’ang’ania katika miji watu wasiojitegemea.

**---------------MWISHO---------------**